

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 232455
Nukushi: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz



Mji wa Serikali – Mtumba,
1 Mtaa wa Ujenzi,
S. L. P. 2888,
40470 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) inafanya ukarabati mkubwa (*Major Rehabilitation*) wa Kivuko MV. Magogoni kinachofanya safari zake kati ya Magogoni na Kigamboni. Zabuni ya ukarabati huu mkubwa umefanywa kwa njia ya ushindani (*International Tendering*) kupitia TANEPS ambapo jumla ya Makampuni mawili yalituma maombi ya kufanya kazi hiyo. Makampuni hayo ni *African Marine and General Engineering Company Limited* ya Mombasa nchini Kenya iliomba kufanya kazi hiyo kwa gharama ya shilingi 7,563,290,100.00 na Kampuni ya *Songoro Marine Transport LTD* ya Mwanza Tanzania ambayo iliomba kufanya kazi hiyo kwa gharama ya shilingi 10,958,197,440.00. Tofauti ya gharama kati ya Kampuni ya *African Marine and General Engineering Company Limited* na Kampuni ya *Songoro Marine Transport LTD* ni Shilingi 3,394,987,340.00. Hivyo, Serikali ilimpa kazi hiyo ya ukarabati mkubwa (*Major Rehabilitation*) Kampuni ya *African Marine and General Engineering Company Limited*. Mkataba wa kazi hiyo ni wa siku 180 sawa na miezi 6. Kivuko MV Magogoni kinachofanyiwa ukarabati mkubwa kina uwezo wa kubeba tani 500 (abiria 2,000 na magari 60).

Kuhusu hoja kwamba gharama ya ukarabati wa kivuko hicho kuwa kubwa ni kwa sababu kimetumika kwa takribani miaka 14 bila ya kufanyiwa ukarabati mkubwa. Sasa hivi ndiyo kinakwenda kufanyiwa ukarabati mkubwa. Katika ukarabati huo zitanunuliwa Injini 5 mpya (Injini 4 zitafungwa kwenye kivuko na Injini 1 ya akiba). Pia, zitanunuliwa na kufungwa *marine steel plates* mpya kwa sababu zilizopo hivi sasa hazifai tena kwa matumizi, *Gear box* mpya, vifaa vya umeme na kielektronik vipya na vifaa vingine.

Baada ya ukarabati huo kukamilika Kivuko hicho kitaweza kutoa huduma kwa miaka 14 au zaidi.

Hapo awali kazi hizi zilikuwa zinatangazwa kwa Makandarasi wa ndani pekee. Mara nyingi Mkandarasi aliyekuwa akipata kazi hizi alikuwa ni *Songoro Marine Transport LTD*. Ushindani wa zabuni kwa Makandarasi wa ndani pekee ulisababisha kutokuwepo kwa thamani ya fedha (*value for money*). Baada ya Serikali kufanya ushindani wa zabuni Kimataifa tumeona uwepo wa thamani ya fedha (*Value for money*) kwa kushuka kwa gharama ya ukarabati wa shilingi 3,394,907,340.00.

Kuhusu *African Marine and General Engineering Company Limited* ni kampuni yenye uwezo wa ukarabati wa Meli, Boti na Vivuko. Kwa mfano Boti za *Azam Marines, Zanzibar 1*, Meli za Zanzibar na meli nyingine mara kadhaa zimekuwa zinakarabatiwa na *Africa Marine and General Engineering Company Limited*.

Kuhusu suala la fedha zinakwenda Kampuni ya *African Marine and General Engineering Company Limited*, ukweli ni kwamba zaidi ya asilimia 75 ya gharama ya ukarabati zinakwenda kwenye manunuzi ya Injini 5 mpya. Vifaa vipya vingine vinavyonunuliwa ni pamoja na *marine steel plates, Gear box*, vifaa vya umeme na kielektronik na vifaa vingine. Vifaa vyote hivyo ambavyo ni vipya vitakavyonunuliwa na Kampuni iliyoshinda zabuni hii (*African Marine and General Engineering Company Limited*) havitengenezwi katika nchi za Tanzania na Kenya. Vifaa na vipuri vyote hivyo vinatoka Nchi za Ujerumani, Dubai, India, Uingereza na nchi nyingine. Hivyo, kiasi kikubwa cha fedha za zabuni hiyo zitatumika kufanya manunuzi ya vifaa tajwa kutoka nchi husika. Aidha, fedha itakayolipwa *African Marine and General Engineering Company Limited* ni ndogo kuliko fedha ambayo ingelipwa kwa mzabuni wa ndani *Songoro Marine Transport LTD* kama kampuni hii ingeshinda zabuni hiyo kwa gharama ya shilingi 10,958,197,440.00

Imetolewa na;

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

21 Februari, 2023